

MBINU ZA UANDISHI

**UAKIFISHI, INSHA, UFAHAMU, UFUPISHO,
MWONGOZO WA JUMLA**

**UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY
P. O. Box 30197
NAIROBI**

Jay Kitsao



NAIROBI UNIVERSITY PRESS

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

YALIYOMO

Shukurani

vii

Utangulizi

ix

Sura ya Kwanza: Uakifishi

1

Utangulizi

1

Umuhimu wa uakifishi katika mawasiliano

2

Viakifishi na Kiuamili

3

Hitimisho

19

Mazoezi

20

Sura ya Pili: Insha

22

Utangulizi

22

Maana ya insha

22

Madhumuni na umuhimu wa insha

24

Mbinu za insha bora

25

Insha bora, hatua kwa hatua

36

Hitimisho

41

SHUKURANI

Wakati nikimenyana na kazi ngumu ya kutayarisha kitabu hiki, nilisika kiwango cha kutumaini na kutamani kwamba nitakapoihitimisha, ningebwaga kalamu juu ya karatasi na kupumua pumuo la kupumzika; lakini kumbe! Hata hivyo, kupuuzilia mbali hii 'kumbe', nashukuru mno kwamba mahusiko yangu katika kazi hii yamenifungulia pazia na kuniangazia uwanja mpana wenze njaa ya kushughulikiwa kwa dhati kitaalamu.

Kuhusu uandishi wa kitabu hiki ambacho nakichukulia kuwa cha kimsingi, nawajibika kuwashukuru watu kadha wa kadha.

Kwanza kabisa namshukuru mwalimu wangu, ustadi, Profesa Mohamed Hasan Abdulaziz, wa Idara ya Ismu na Lughu za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi. Waama bila ushauri na himizi zake za kitaalamu kwangu katika kila ninachoazimia na kujaribu kuandika kiusomi, haiyumkiniki kuwa ningefika mbali sana katika kumakinika na kujiamini namna ninavyojichukulia sasa.

Pili, sisiti kumtaja Ustadhi Daniel Mkude, wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tangu tulipokutana mwaka wa 1978, Profesa Mkude amekuwa akinishauri na kunihimiza niandike kazi za kitaalamu pia, mbali na zile za kisanaa tu, ambazo nimewahi kuziandika. Namshukuru mno kwa jinsi ambavyo daima amekuwa akinifanya njiulize, *Kwa nini ananiambia hivi? Niandike juu ya nini?*

Tatu, nawashukuru wahadhiri wenzangu wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaamu. Hawa ni Prof. Ndugu Euphrase Kezilahabi na Ndugu F.E.M.K. Senkoro. Ndugu hawa wamekuwa wakinikabidhi au kuni peleke vitabu na makala *yao* ya kitaalamu kila ilipowezekana. Bila wao wenye we kuelewa pengine, vitabu na makala *yao* daima zilikuwa zawadi au tunu zilizonifikia pamoja na ujumbe nilioufasiri kuwa *wenzako wanachangia utaalamu, wewe unafanya au unangojea nini?*

Nne, sitakuwa natenda haki nisipowataja wahadhiri wenzangu katika somo la Stadi za Mawasiliano ya Kiswahili - Dkt. Mohamed Bakari na Marehemu Bw. Kadenge Kazungu, katika Idara ya Ismu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi. Hawa pia nawashukuru kwa dhati kwa jinsi ambavyo walikuwa tayari kunipokea kila mara na kunivumilia katika majadiliano juu ya masuala mbalimbali ambayo nilihitaji kuyaelewa vizuri.

Pia nawashukuru maafisa fulani wa Baraza la Mitihani la Kenya (BAMITAKE) na wale wa Taasisi ya Elimu ya Kenya (TAEKE) kwa kunihimiza niandike kazi ya kitaalamu kuhusu insha, usupisho, na usahamu.

Nashawishika kuwataja wanafunzi wangu wa kiwango cha M.A: Mwenda A. Mbatia, Ayubu Mukhwana, Timammy Rayya, Naomi L. Shitemi, na Peter Karanja kwa mijadala na mirahano ambayo illichimbua chimbua na kuweka wazi masuala na masiala ya kimsingi katika mada nilizoziandikia. Nachukua nafasi hii pia kuwatakia kila la heri na mafanikio katika juhudhi zao za kujiingiza na kujiunga na ulimwengu wa usomi na utaalamu.

Nachukua fursa hii pia kumshukuru kwa dhati za moyoni mke wangu mpenzi, Bi. Julia W. Kitsao, na jamii yangu kwa jumla kwa jinsi walivyonivumilia wakati wote nilipokuwa 'mbali' nao nikitayarisha kazi hii. Ulikuwa wakati mgumu ambapo hata maongezi kati yetu yalikuwa haba, na ya hali kama vile ya kuvumiliana tu. Mara nyingi nilihitaji kuwa peke yangu kabisa - mimi na tafakari zangu tu. Hata kuambiwa tu kwamba chakula kilikuwa tayari kulikuwa kusumbuliwa na kupotezewa wakati niliouthamini mno. Mama watoto alipopata wasaa kidogo nami, akaninong'onezea kwamba nimegeuka kuwa mgeni nyumbani kwangu! Na jambo hilo aliniambia kwa tahadhari kwani hasira zilikuwa zikinipanda na kuniponyoka ovyoovyo kama vile nyigu hata kabla hawajachokozwa.

Mwisho, lakini si mwisho kwa umuhimu, namshukuru Bi Getrude S. Mwaeni kwa kupiga chapa kazi yote hii wakati nilipomtaka kufanya hivyo na jinsi nilivytaka.

Jay Kitsao

Januari, 1995

UTANGULIZI

Mbinu za Uandishi ni matokeo ya hamasa au ghera, yaani dukuduku la ndani kwa ndani kwangu. Msukumo wenyewe ni zao la kero kwamba ijapokuwa Kiswahili kinafundishwa kama taaluma katika asasi za kielimu kwingi ulimwenguni, baadhi ya nyanja zake za ufundishaji hazijashughulikiwa kikamilifu kinadharia.

Wataalamu wengi wamejihusisha zaidi na masiala hasa ya kisarufi kama kwamba kuna mapya sana ya kuongelea katika kipengee hiki. Wengine wamejishughulisha na nadharia za uchambuzi na uhakiki wa fasihi kulingana na maudhui na matumizi ya lugha. Mwelekeo huu bila kurekebishwa mapema ungemaanisha hali kama vile baharini ambamo samaki na viumbwe wengine ni wengi, lakini wavumao na kujulikana ni wachache tu. Jambo hili lina hatari ya kwamba utaalamu haupigi hatua - haumong'onyoi ardhi mpya, wataalamu wetu wakishindana kwenye uwanja finyu, kila mmoja akijitahidi kuona kwamba anatajika kutokana na kujaribu kuyaandaa bora yale ambayo yashawasilishwa tayari.

Pia, ari iliyonihimiza niandike nadharia hii ilitokana na tajriba ya miaka mingi ya uhadhiri kwenye ngazi mbili katika chuo kikuu. Kwanza, katika kufundisha stadi za mawasiliano ya Kiswahili katika kiwango cha shahada ya B.A., niliwajibika kuingilia kinadharia na kwa undani mahusiko ya uakifishi, insha, ufahamu, na ufupisho. Pili katika kiwango cha M.A., nilifurahia mijadala iliyozusha masuala fulanifulani muhimu na ya kimanusaa kuhusiana na mada hizi.

Fauka ya tajiriba yangu kutokana na uhadhiri, nilibahatika kupata ile heshima nadra, yenyе manufaa makubwa, ya kuombwa ushauri wa mara kwa mara kuhusu mkondo unaosaa kuchukuliwa na mahusiko ya kazi hif. Ni katika wasaa huo ambapo pia niliweza kuzama katika mijadala iliyofungua bongo kuhusu masiala fulanifulani ambayo nilikuwa sijayafikiria barabara kabla.

Kazi hii imetayarishwa kwa manufaa ya waalimu, wanafunzi, na wale wote wanaojali au wanaohitaji kujiendeleza kimawasiliano kwa matumizi ya lugha. Kimsingi, kozi hii ni kuhusu matumizi yafaayo ya uakifishi, uandishi wa insha bora, matarajio ya usahamu kama somo, na utayarishaji wa usupisho. Lakini madhali masiala yanayomulikwa na kushughulikiwa ni ya kiistilahi kulingana na mahitaji ya kimasomo, itakuwa ya manufaa zaidi hasa kwa waalimu na wanafunzi wa shule za upili pamoja na wanafunzi na wahadhiri vyuoni.

Insha, usahamu na usupisho ni masomo muhimu katika viwango vyote vya asasi za kielimu kote ambako Kiswahili kinafundishwa kama taaluma. Lakini kinyume cha matarajio ni kwamba masomo haya hayajatolewa nadharia ya kueleza hatua kwa hatua jinsi waalimu pamoja na wanafunzi wanavyofaa kuyashughulikia. Ni jambo lisilobishika kwamba uakifishi una mengi yaliyoandikwa juu yake. Waalimu na wanafunzi wao kwa jumla wana marejeo kuhusu matumizi bora ya viakifishi. Udhuru wa kuhusisha uakifishi katika mwongozo huu ni kuurejelea kama kumbukumbu muhimu ya mbinu ya kimsingi inayofaa kuzingatiwa kwa stadi zote tatu

Ni kweli waalimu wanaojali wanafunzi wao hujitahidi kujikunakuna vichwa au hata kujaribu wavezavyo kupata mwangaza kutokana na vitabu vilivyoandikwa hasa kwa Kiingereza, ili angalau wapate maelezo thabiti zaidi ya kuwasilisha darasani. Lakini madhali kazi zao sanasana hunuiwa kuhudumia mahitaji ya hapo kwa hapo, zinakuwa za kijujuu tu. Hazipai na kusikia viwango vya utaalamu unaostahili kuhifadhiwa kwa manufaa na matumizi ya waalimu na wanafunzi kwingineko. Kazi hii imeandaliwa kwa dharura na madhumuni ya kuziba pengo hilo.

Kwenye vitabu vilivyoandikwa kwa lugha za kigeni kuhusu masuala ya insha, usahamu na usupisho, inatokea kwamba insha iwe imeshughulikiwa katika kitabu kimoja, usahamu katika kingine, na usupisho hali kadhalika kwingineko. Jambo hili lamaanisha kwamba mwalimu anapoteza wakati katika kusikiria

na kutafuta ni wapi akimbilie ili apate mada ipi. Kitabu hiki kinakinga dhidi ya sumbuko hilo.

Kufikia hapa tunaweza kusema kuwa kazi hii inajivunia mambo mawili. Moja, ndiyo ya kwanza na ya kipekee katika lugha ya Kiswahili kama taaluma masomoni kwenye uwanja tasa hasa kuhusu nadharia ya mahusiko yake. Pili, ndiyo ya kwanza pia kwa lugha ya Kiswahili katika kushughulikia mada zinazohusika kwenye kusanyo moja.

Matumaini ni kuwa kazi hii itaenda mbali katika kuhudumia mahitaji ya uandishi bora wa insha, uelewekaji mzuri wa ufahamu, na usupisho ifaavyo wa makala mbalimbali.

Nawajibika kusema kwa msisitizo kuwa si madhumuni ya kazi hii kufundisha lugha ya Kiswahili kisarufi au kimtindo. Inachukulia kuwa hadhira tayari ina ujuzi wa kutosha kuhusu masiala haya ya kimsingi. Yaani uchukulizi ni kuwa hadhira tayari ishajifunza au ishafunzwa Kiswahili cha kutosha kiutendaji, na kilichobaki ni upalilizi tu wa ujuzi unaohitajika ili kujenga jina katika uandishi.